

# HADITHI! HADITHI!

## KWA NINI JUA NA MWEZI HUISHI ANGANI

Hapo zamani za kale, jua na maji walikuwa marafiki wakubwa sana. Wote waliishi hapa duniani kwa pamoja. Kwa siku nyingi, jua lilimtembelea maji lakini maji hayakuwahi kumtembelea. Wakati mmoja jua aliamua kumuuliza maji, mbona hakuwahi kumtembelea nyumbani mwake. Maji naye akamjibu ya kwamba alihofu kuwa nyumba ya jua haikuwa kubwa ya kutosha, na kwamba kama yeze angekuja pamoja na watu wake, hawangeweza kutoshea kwa nyumba moja.

Hatimaye, maji alimwambia na kumuonya jua, "Kama ungetaka nikutembelee, lazima ujenge nyumba kubwa sana. Kwa maana watu wangu ni wengi sana na huchukua sehemu kubwa ya nyumba."

Jua aliahidi maji kuwa atafanya alivyoagiza na kujenga kiwanja kikubwa. Baadaye jua alirudi nyumbani kwa mke wake, mwezi, ambapo alimsalimia kwa tabasamu alipokuja kumfungulia mlango. Alimwambia mke wake, mwezi, yale aliyoahidi maji, na siku ya pili akaanza kujenga eneo kubwa ili kumkaribisha rafiki wake wa dhati.

Mwishowe, ujenzi ulimalizika, jua alimuuliza rafiki yake aje amtembelee siku iliyofoata.

Wakati maji alipowasili jioni, alimwita jua kwa umbali na kumuuliza kama ingekuwa salama aingie chumbani, naye jua akajibu, "Naam, kuja, rafiki yangu."

Maji kisha akaanza kutiririka chumbani, akifuatana na samaki na wanyama wote wanaoishi katika maji. Alipofika urefu wa magoti ya binadamu, alimuuliza jua kama ilikuwa salama bado yeze na watu wake kuingia. Jua naye akawahimiza waendelee kuingia.

Maji yalipofika urefu wa kichwa cha mtu, maji alimuuliza jua tena, "Je, unataka zaidi ya watu wangu kuja?" naye jua na mwezi wote akamjibu, "Naam," bila kujua lolote bora. Maji yaliendelea kujaa hadi ikawabidi jua na mwezi kukaa juu ya paa lao.

Kwa mara nyingine, maji alimuuliza jua na mwezi kama ilikuwa salama kuingia tena na kupokea jibu lile lile kutoka kwao. Hatimaye, maji yalifurika kwa haraka hadi juu ya paa. Jua na mwezi walilazimwishwa kukimbilia juu angani ambapo wanaishi hadi leo.

### **JINSI NDOVU ALIVYOPATA PUA NDEFU**

Hapo zamani za kale ndovu alikuwa na pua ndogo. Ilifanyika kuwa mwaka mmoja, mvua haikunyesha kwa miezi mingi. Mabwawa na maziwa yalianza kukauka, na mito ya maji ilikuwa kidogo sana na kufanya wanyama wote msituni kuwa na kiu sana. Siku moja, ndovu aliamua kwenda kutafuta maji kwenye mto uliokuwa karibu na msitu.


Pale mtoni paliishi mamba mkali mwenye rangi ya zambarau. Mamba yule alipomwona ndovu anakaribia mtoni, alipaza sauti na kumwambia, "Rudi ulikotoka, maji tayari ni kidogo hapa mtoni. Ukinywa, nitabaki na nini mimi? Ndovu yule alielewa kuwa ni hatari kupigana na mamba, kwa hivyo aliamua kwenda na kurejea baadaye wakati ambapo, mamba angekuwa usingizini.

Katika mto huo, aliishi chura mwenye rangi ya zambarau. Kila mara mamba alipokuwa akiogelea, chura aliruka mgongoni mwake, jambo ambalo halikumfurahisha mamba. Mamba alijaribu kutingiza mwili wake ili chura aweze kuanguka, bila mafanikio. Chura naye kushuhudia haya, angeangua kicheko kikubwa.

Siku moja , mamba alikuwa anapumzika kwenye jiwe kubwa. Ndovu alichukua fursa hii na kusogea kimya mtoni na kuanza kunywa maji. Pindi tu, chura aliruka kwenye mgongo wa mamba , na kumwamsha. Kwa hasira nyingi, mamba alianza kuogelea kando ya mto huku akitingisha mwili wake kwa ukali ili kujikwamua kutoka kwa chura lakini chura naye hakuyumba.



Muda si muda, mamba alimwona ndovu. " Mbona unathubutu kunywa maji katika mto wangu baada ya kukuonya?" alimkemea ndovu kwa hasira. Kwa vile hakuweza kujikwamua kutokana na chura, alielekeza hasira yake yote kwa ndovu. Alimshambulia ndovu kwa ghafla na kukamata pua lake na kuanza kumvuta ndani ya mto.



Maskini ndovu alianza kusihi kwa kilio, "  
Pua langu laumia.. niachilie niende zangu...  
sitarudi kunywa maji haya tena." Lo!  
Mamba alifunga masikio ndi wala hakusikia  
kilio chake ndovu.

Hatimaye, kwa nguvu na kishindo, ndovu alijivuta na kufaulu katika kulikomboa pua lake kutoka kinywa cha mamba, lakini kwa sababu ya ule mvutano, pua la tembo lilirefuka zaidi. Ndovu alijazwa na hasira na kunywa maji yote ya mto ule. Kisha alichukua matope na kuwamwagilia chura na mamba. Kwa vile maji yalikwisha, hawangeweza kusafisha miili yao kutohana na matope. Tangu wakati huo, ndovu wana pua ndefu, na mamba na chura hawana rangi za zambarau tena.